

## Somo la kwanza: Nini maana ya Vifaa saidizi ?


- Vifaa saidizi ni vifaa vinavyotumiwa na watu kufanya kazi ambazo wasingeweza kuzifanya vizuri ama wasingeweza kuzifanya kabisa kama wasingetumia vifaa hivyo.
- Vifaa saidizi vinaweza kutumiwa na watoto pamoja na watu wazima.
- Kuna aina mbalimbali za vifaa saidizi ambavyo zinaweza kusaidia watu katika maeneo mbali mbali ya maisha yao . Kwa mfano: kufikiria, kuwasiliana, kusikiliza, kuona na kwenda maeneo mbali mbali, pamoja kujihudumia.
- Watu wengi wanatumia zaidi ya kifaa saidizi kimoja, kulingana na mahitaji yao

## Somo la pili: Nani anahusika kwenye utoaji wa vifaa saidizi?

- Watu wengi wana jukumu la kugawa vifaa saidizi. Watu hawa ni pamoja na:
  - Mtu anayehitaji kutumia kifaa saidizi
  - Familia na marafiki za watu wanaotumia vifaa saidizi
  - Watu ambao wanaelekeza wahitaji sehemu ya kupata huduma ya vifaa saidizi
  - Watoa huduma ya Afya waliopata mafunzo
  - Wanajamii

## Somo la tatu: Utaratibu wa kugawa Vifaa saidizi

Vifaa saidizi vinagawiwa kwa kufuata hatua nne:



- Hizi hatua zinasaidia kuhakikisha kuwa watumiaji wa vifaa saidizi wanapata vifaa ambavyo ni salama na stahiki; na wana stadi za kuvitumia na waendelea kupata msaada ili kuhakikisha kuwa vifaa hivyo vinaendelea kukidhi mahitaji yao
- Ni muhimu sana mtu atakayepata kifaa saidizi (na familia yake au mtu anayemhudumia) kuwa kushiriki kikamilifu kwenye kila hatua ya mchakato wa kupata kifaa saidizi

## Somo la nne: Mambo ya kuzingatia wakati wa utoaji wa huduma ya vifaa saidizi

- Wakati mwingine vifaa vyaweza hutolewa kwa haraka na wakati mwingine inaweza kuchukua muda mrefu kugawa kifaa saidizi kwa mhusika. Hii inaweza kutokana na mambo kadha wa kadha:
  - Namna (ugumu) kifaa saidizi kilivyo
  - Mahitaji na hali ya afya ya mhusika.
  - Mazingira ambayo mhusika atatumia kifaa saidizi.
  - Uzoefu wa mhusika ambaye atatumia kifaa saidizi.
- Mara nyingi watumiaji hupata vikwazo katika kufanya kile wanachotaka kufanya, pamoja na kuwa na vifaa saidizi muafaka, Baadhi ya vikwazo hivi ni pamoja na:
  - Vikwazo vya kimazingira kama vile eneo lisilofikika kiurahisi
  - Unyanjapaaji na Ubaguzi
  - Ukosefu wa taarifa
  - Kutokuwepo sera na huduma zinazohusu utoaji wa huduma za vifaa saidizi.
- Kila mmoja ana jukumu la kufanya ili kuhakikisha kuwa watu wanaotumia vifaa saidizi wanashirikishwa kwenye shughuli za kijamii na wanaweza kufanya vitu ambavyo wanataka kufanya kama watu wengine amabo hawahitaji vifaa saidizi.